# Watoto katika kilimo cha wakulima wadogo wa nchi za Tanzania




Pamba Izalishwayo Afrika

# Utangulizi

Mpango wa Pamba izalishwayo Africa (CmiA) una lengo la kuboresha hali ya maisha ya wakulima wengi wa pamba katika Africa, pamoja na makampuni yanayotekeleza kilimo cha pamba kupitia mradi wa (COMPACI), “Mradi wa Pamba izalishwayo Africa” una hakikisha kuwa kilimo cha pamba kinakuwa na kuwa endelevu, Inafuata 3P yaani People (Watu) - Profit (Faida) - Planet (Mazingira) ina maanisha, Jamii, Uchumi na Mazingira.

Katika viwango endelevu, Mradi wa Pamba izalishwayo Afrika (CmiA) inaonyesha uhusisishi mbaya wa watoto katika shughuli mbalimbali hasa zile za kilimo, kama ilivyoelezwa kwenye kanuni za Shirika la kazi Duniani ILO kifungu 138 na 182 imekatazwa na hairuhusiwi watoto kujihusisha na kazi nzito isipokuwa kazi zile tu ambazo hazina madhara kwa Afya zao, Usalama, Ustawi wao, Elimu yao na maendeleo yao kwa ujumla, pia katika kazi hizo ni lazima wasimamiwe na watu wazima na wapewe mafunzo stahiki.

Katika vielelezo vya picha inaonyesha jinsi watoto wanavyoshiriki katika kilimo cha pamba katika familia za wakulima wadogo katika nchi za Tanzania. Picha hizo zimeandaliwa ili kuhamasisha wadau wa uzalishaji wa pamba hasa wazalishaji ambao wanahitaji nguvu kazi ya ziada katika shughuli mbalimbali.

Mpangilio wa picha kwa mbele na maelezo kwa nyuma inamuwezesha (Mkufunzi /Afisa ugani) kufikisha ujumbe unaokusudiwa kwa wakulima, Vipindi vya mafunzo vitafanyika kwa njia ya ushirikishwaji

Mpango uliopendekezwa wa Maswali na Majibu unasaidia kumuelekeza mkufunzi namna mzuri ya kufundisha.

AID BY TRADE FOUNDATION

COTTON MADE IN AFRICA

# Jinsi Ya Kutumia Picha Katika Mafunzo

Kijarida cha Picha ni nyenzo inayotumika wakati wa vipindi vya mafunzo ambayo inaonyesha picha mbalimbali, hii inaonyesha picha kwa upande wa mbele na maandishi kwa nyuma inamuwezesha mtumiaji (Mkufunzi au Mtaalamu wa kilimo) kufikisha ujumbe mahususi kwa njia ya ushirikiswaji

Mkufunzi anaanzisha majadiliano miongoni mwa washiriki yanayoendeshwa kwa njia ya maswali na majibu, Ujumbe unaopangwa kufikishwa utaeleweka vizuri Zaidi kwa njia ya maswali na majibu yatakayo wekwa kwenye kijarida.

Wakati wa mafunzo Taswira za picha zitaonyeshwa (Moja baada ya nyingine) kwa washiriki watatafsiriwa na kujadili shughuli zilizoonyeshwa kwenye picha ili washiriki waweze kuelewa umuhimu wa mada inayojadililiwa.

Maswali na Majibu yanayopendekezwa yanatumika kama mwongozo kwa mkufunzi Kama majibu ya washiriki hayaleti ujumbe unaokusudiwa, Mkufunzi atauliza washiriki maswali ya mwongozo ili kuwaongoza washiriki kwenye lengo lililokusudiwa.


Maswali hayo yanaweza kuulizwa kama Nani/Nini/Lini/Wapi/Kwanini pamoja na taarifa zinazofanana. Maswali na Majibu yatumike kama mwongozo wa mkufunzi na haitakiwi kusomwa mara kwa mara wakati mafunzo yanaendelea. Baada ya kujadili picha maalumu na kupitia maswali, Muulize mmoja wa washiriki aweze kutoa maelezo kwa kifupi kuona kama mafunzo na ujumbe uliotolewa kwa njia ya picha umeeleweka, pia picha zinazofuata zitajadiliwa kwa njia hiyohiyo.
Wape muda washiriki waziangalie picha kwa makini na kuzitafakari, ishirikishe washiriki wengi Zaidi.


Kila picha iambatane na ukurasa unaomshabihi mkufunzi, Hakikisha una ukurasa wenye maswali na majibu ikiwa na ujumbe mahususi kwa lugha ya Kiswahili.

Hadithi inayosimuliwa kwa njia ya picha inahusisha familia 2 za wakulima wa pamba ambao ni Masanja na Shija.


| **FAMILIA (Upande wa kushoto)** | |
|---|---|
| Baba | *Masanja* |
| Mama | *Janet* |
| Mtoto mkubwa wa Kiume (15) | |
| Mtoto mkubwa wa Kike (13) | |

| **FAMILIA (Upande wa Kulia)** | |
|---|---|
| Baba | |
| Mama | |
| Mtoto mdogo wa Kike (14) | |
| Mtoto mkubwa wa Kiume (10) | |


A
COTTON
MADE IN
AFRICA


B

# Picha Na 1




**Swali:** **Unaona nini kwenye picha A?**

**Jibu:** Tunaona Familia ya Masanja na Janet. Nyumba yao ni mzuri imeezekwa kwa bati, Wana maksai anayesaidia shughuli mbalimbali, wamevaa nguo mpya na za kupendeza, Katika familia yao wana watoto 5: Mussa, (Miaka, 20, anayefanya kazi mjini), _________(Miaka, 15), _____________ (Miaka, 13), ______________ (Miaka, 6) na Mtoto mdogo. Watoto 3 yaani ________________, _______________ na _________________wanaonekana wamevaa sare za shule.

**Swali:** **Unaona nini kwenye picha B?**

**Jibu:** Tunaona familia ya Shija na Mariam. Nyumba yao ni ya kawaida na imeezekwa kwa nyasi, Hawana maksai, wamevaa nguo zilizochakaa. Wana watoto 4: _______________ (Miaka, 20, hana kazi ya kuajiriwa anaishi mjini), ______________ (Miaka, 14), Kijana wa makamo _________________ na pia wana Mtoto mdogo, ________________ na _____________________ hawaendi Shuleni, huwa wanakwenda kufanya kazi za shamba.

***Ujumbe:*** *Familia hizi mbili zilianza maisha kwa wakati mmoja, lakini kupitia mafunzo, Elimu, Elimu ya uhasibu, na kanuni bora za kilimo cha pamba familia ya Masanja katika Picha A ameweza kuboresha maisha katika ngazi ya familia, Mfumo wa maisha ya Shija unaendelea kutumia watoto katika shughuli mbalimbali za kilimo na watoto hawaendi shuleni. Chini ya mradi wa pamba inayozalishwa Afrika (CmiA) na sheria ya nchi inawataka wazazi kupeleka watoto shule.*


PRIMARY AND SECONDARY SCHOOL
COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 2



**Swali: Unaona nini upande wa KUSHOTO wa picha?**

**Jibu:** Watoto wa Masanja wana mpungia baba yao mikono wanapoelekea shuleni.

**Swali: Kwanini ni jambo zuri kupeleka watoto shule?**

**Jibu:** Watoto wakipelekwa shule watapata nafasi ya kujifunza Kusoma, Kuandika na kuhesabu, Hii inawapa upeo mkubwa katika maisha yao, pia itawawezesha watoto kuwasaidia wazazi wao kusoma majarida mbalimbali ya kilimo bora, Kufanya mahesabu yanayohusisha gharama za kilimo, na mbinu mbalimbali zitakazo wawezesha kusimamia vema shughuli zao za kilimo, Watoto watawasaidia wazazi wao kusoma Mikataba, Barua, Vipeperushi vya matumizi bora ya viuatilifu / viuadudu.

**Swali: Unaona nini upande wa kulia wa picha?**

**Jibu:** Shija na Mariamu na watoto wao wawili wamebeba majembe wanakwenda shambani kufanya kazi.

**Kuna matatizo gani yanaweza kutokea kwa kuwapeleka watoto kufanya kazi za**

**shamba badala ya kuwapeleka shule?**

**Jibu:** Inawakosesha watoto kupata fursa ya kusoma na kuandika, pia familia haipati fursa ya kufanya kilimo bora kwani hakuna mwanafamilia anayeweza kusoma majarida ya kilimo bora na kufanya mahesabu ya gharama za uzalishaji na hata wakati wa masoko.

***Ujumbe:*** *Kupeleka watoto shule kunawapa fursa ya kupata maisha bora kwa siku za usoni.*


COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 3



**Swali: Unaona nini kwenye picha hii?**

**Jibu:** Ni asubuhi watoto wa familia ya Masanja wanakwenda shuleni baba yao analima wakati mama yao anasambaza mbolea ya mboji shambani iliyowekwa kwenye mifuko

**Swali: Wazazi kwa maana ya Masanja na Janet wanafanya nini na mbolea ya mboji:**

**Jibu:** Wanarutubisha ardhi kwenye shamba lao, Masanja anatawanya mboji juu ya udongo ili iweze kuchanganywa wakati wa kutifua udongo, mboji ni nzuri kwa kurutubisha udongo na ni ya gharama nafuu ukilinganisha na mbolea za viwandani kwani masalia ya mimiea yatumikayo kutengeneza mboji hayauzwi.

**Swali: Wazazi Kwanini watoto hawahusiswi kufanya kazi za kulima na shughuli nyingine za shamba kama wafanyavyo wao?**

**Jibu:** Kwasababu hizi ni kazi ngumu zinazochukua muda mrefu na zinafanywa na watu wazima tu, watoto nafasi yao ni shuleni wakiwa na wanafunzi wenzao.


COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 4



**Swali: Unaona nini kwenye picha hii?**

**Jibu:** Shamba la pamba linaonekana likiwa na miche mingi kuliko inavyotakiwa inahitaji kupunguzia, Inaonekana wanafamilia wanajishughulisha na kupunguzia mimea.

**Swali: Je watoto wanaweza kufanya kazi ya kupunguzia miche?**

**Jibu:** Kupunguzia miche siyo kazi ya hatari na yenye athari kwa watoto, watoto wanaweza kuwasaidia wazazi wao kupunguzia miche mashambani baada ya muda wa shule, wakati wa mapumziko ya mwisho wa wiki au wakati wa likizo, Watoto wakubwa wanaweza kusaidia kazi ya kuchunga mifugo na kuhakikisha hawaharibu mazao.



# Picha Na 5



**Swali: Unaona nini kwenye picha hii?**

**Jibu:** Masanja anachanganya dawa kwa ajili ya kupulizia kwenye shamba, amevaa vifaa maalumu kwa ajiili ya kupulizia dawa kama anavyoonekana (ovaroli viatu vya buti, Kofia, Miwani kubwa ya kukinga macho, Glovsi, na kifaa cha kuziba mdomo na pua (maski) Kama hauna ovalori unaweza kuvaa suruali ndefu na shati la mikono mirefu inaweza kukusaidia usipate madhara.

**Swali: Kwanini tunavaa nguo na vifaa maalumu vya kujikinga wakati wa kupuliza dawa?**


**Jibu:** Viuatilifu vina sumu kali sana ambazo ni hatari kwa afya, Watu wazima tu ndiyo wanaoruhusiwa kufanya shughuli ya kupulizia na wachukue taadhari kubwa.

**Swali: Je baada ya kupiga dawa Masanja anazifanyia nini chupa tupu?**

**Jibu:** Masanja huiharibu kwa kuikatakata chupa iliyotumika na kasha kuichimbia kwenye shimo ili watoto wasije wakachezea au kuweka kitu chochote, pia chupa iliyotumika hairuhusiwi kutumika tena.

**Swali: Je watoto wanaruhusiwa kufanya kazi ya kupulizia viatilifu kwenye pamba?**

**Jibu:** Hairuhusiwi kabisa Viuatilifu ni hatari sana kwa watoto na vijana wadogo kwa sababu wanaendelea kukua, ________________ ambaye hajafikisha umri wa miaka 18 anapeleka maji lakini haruhusiwi kukaribia eneo hilo, Masanja anamuamuru __________________ aondoke eneo la shambani, Upuliziaji wa viuatilifu hauruhusiwi kwa wakinamama wanyonyeshao na wajawazito.


COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 6




**Swali: Unaona nini kwenye picha hii?**

**Jibu:** Masanja amemaliza kupulizia viuatilifu na ameondoka shambani kuelekea nyumbani, amechimbia kwenye shimo chupa za viuatilifu zilizo tumika, anahifadhi vifaa vya kupulizia dawa kwenye sehemu yenye kivuli na yenye hewa ya kutosha ambapo pamezungushiwa uzio na mlango imara wenye kufuli na iko mbali na shamba.


**Swali: Kwanini Masanja haifadhi viatilifu kwenye makazi yake?**

**Jibu:** Viatilifu ni sumu kali sana, Kila kitu kilichotumika katika kupulizia viatilifu ikiwemo nguo alizovaa lazima vihifadhiwe kwenye eneo lililojitenga na ambalo watoto hawawezi kufika, Masanja atajishafisha kwa maji safi pamoja na vifaa vyote vilivyo tumika katika zoezi la Upuliziaji Viatilifu.

**Swali: Je Mke wa Masanja na watoto wake wanafanya nini?**

**Jibu:** Janet mke wa Masanja na watoto wamebaki nyumbani hawakwenda kwenye shughuli ya upuliziaji viuatilifu, Janet ana andaa chakula akisaidiwa na binti yao ___________________, ______________________ anawapatia chakula kuku na ___________________ anacheza mpira, watoto wanaweza kuwasaidia wazazi wao kazi nyingi tofauti kama vile: Kulisha kuku, Kuokota mayai kwenye mabanda ya kuku, Kusaidia kupika chakula, kuhudumia bustani ya mboga na maua, kuosha vyombo n.k

***Ujumbe:*** *Viuatilifu na shughuli mzima ya upuliziaji wa viuatilifu ni hatari nas siyo salama hivyo basi inatakiwa vihifadhiwe mbali na maeneo yanayoweza kufikiwa na watoto, Kama kibanda kilichoko kwenye picha hakiwezi kujengwa, itabidi viuatilifu vihifadhiwe sehemu iliyofungwa na yenye usalama.*


COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 7



**Swali: Unaona nini kwenye picha hii?**

**Jibu:** Picha inaonyesha kazi ambazo watoto wanaweza kuwasaidia wazazi wao nje ya maeneo ya makazi yao kwa mfano baada ya muda wa shule wanaweza kupeleka mifugo malishoni,wanaweza kuwapeleka mifugo maeneo ya mbali wakati wa shughuli ya kupulizia viuatilifu shambani, wanaweza kuchota maji, kutafuta kuni, kuvuna mazao kama vile maembe, machungwa, na karanga pia wanaweza kuwasaidia wazazi kupeleka mazao sokoni kwa ajili ya kuuza.

**Swali: Mapambano dhidi ya ajira zenye athari kwa watoto ina maana ni kuwafanya watoto wawe wavivu na wasiwasaidie kazi wazazi wao?**

**Jibu:** Hapana watoto wanaweza kusaidia familia kuongeza kipato bila kuhatarisha afya zao na maendeleo yao kwa ujumla ni muhimu kwamba kuwepo na uwezekano wa watoto kwenda shule.


COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 8



**Swali: Unaona nini kwenye picha hii?**

**Jibu:** Huu ni msimu wa pamba Masanja na Janet wanavuna pamba.

**Swali: Je watoto nao wanawasaidia wazazi wao kuvuna pamba?**

**Jibu:** Kipindi baada ya muda wa shule, ______________________ anawasaidia anapopata nafasi, Kwenye kivuli anaonekana ___________________ na _____________________ wanasaidia kuchambua pamba yaani wanaondoa vipande vya plastiki, majani, na nyasi. Pamba inayovunwa kwa mkono ni safi kuliko pamba inayovunwa kwa mashine kwasababu ni rahisi kuondoa takataka kwa mkono kuliko mashine. Kuchambua ni kazi inayoweza kufanywa na watoto.

***Ujumbe:*** *Kuvuna pamba ni kazi inayoweza kufanywa na watoto baada ya muda wa shule, siku za mwisho wa wiki, au wakati wa likizo lakini kazi hii inatakiwa kufanywa katika mazingira yasiyo na usumbufu, manyanyaso au vikwazo vya aina yeyote ile.*


COTTON
MADE IN
AFRICA

# PICHA NA 9




**Swali: Unaona nini kwenye picha hii?**

**Jibu:** Shamba la Masanja linaonekana mkono wa kulia na shamba la Shija mkono wa kushoto, Masanja amepata mavuno mengi Zaidi ya Shija ingawa Shija ametumia muda mwingi shambani na watoto wake.

**Swali: Kama watoto wa Masanja wamekuwa wakitumia muda mwingi shuleni na wamekuwa**

**Jibu:** Masanja amepata mavuno mengi kwa sababu aliweza kutumia mbolea ya mboji kwenye shamba lake pia amekuwa akipulizia viuatilifu pale tu ambapo ilikuwa ni lazima kutumia kwa jinsi hiyo ameweza kupunguza gharama za uzalishaji, Watoto wa Masanja hawakuwa wavivu au hawakupoteza muda kwa kwenda shuleni bali wameweza kujifunza vitu vingi ambavyo vimekuwa msaada mkubwa sana kwa wazazi wao kwa mfano wanaweza kusoma taarifa zinazohusiana na matibabu ya mifugo yao, taarifa za masoko au maelekezo yanayotolewa na maafisa ugani.

**Swali: Nini kilichosababisha Shija asipate mafanikio?**

**Jibu:** Shija hakutumia mbinu bora za kurutubisha shamba lake, ametumia pesa nyingi kununua viuatilifu na ametumia viuatilifu hata wakati ambao vilikuwa havihitajiki kwa jinsi hiyo wadudu waharibifu kama funza wa vitumba na katapila waliweza kuharibu mimea ya shamba lake na kusababisha kuwa na mavuno kidogo. Kwa vile Shija hawezi kusoma na kuandika ilikuwa vigumu kufuatilia mafunzo anayopewa na Maafisa ugani pia kwa vile na watoto wake hawajui kusoma wala kuandika hawawezi kutoa msaada wowote, kwa jinsi hiyo familia ya Shija haikuwa na nafasi ya kupata maendeleo.

***Ujumbe:*** *Watoto wanaokwenda shule siyo wavivu bali wanapata makuzi mazuri na mafanikio endelevu na anachangia faida ipatikanayo kwenye familia.*


COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 10



**Swali: Masanja anaonekana anafanya nini?**

**Jibu:** Masanja anauza pamba yake kwa kampuni inayonunua pamba na wanaume wanaonekana wanapakiza magunia yaliyoshindiliwa pamba kwenye gari, Masanja yuko sokoni kwa ajili ya kutoa msaada.

**Swali: Watoto wanaonekana wakifanya nini?**

**Jibu:** Watoto wamefuatana na wazazi wao kwenye sokoni kushuhudia Kinachoendelea na wanasaidia wazazi wao kupiga mahesabu, na kusoma mikataba inayohusu masoko, wakati mtoto mdogo anaonekana anaendelea kucheza.

**Swali: Je watoto wanaweza kubeba magunia yaliyoshindiliwa pamba?**

**Jibu:** Hapana hairuhusiwi kabisa watoto kubeba mizigo kwani inaweza kuleta madhara makubwa kwenye mfumo wa afya zao.

***Ujumbe:*** *Msimu wa masoko ya Pamba ni muhimu sana kwa wakulima wote na kwa familia kwa ujumla matumizi bora ya pembejeo huleta mavuno mazuri, hii inamaanisha mapato mazuri kwa mwaka mzima.*


COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 11




**Swali:** **Je Masanja na Familia yake wanafanya nini?**

**Jibu:** Masanja na familia yake wanapumzika wanatafakari mapato waliyoyapata katika msimu huu kutokana na walivyozalisha pamba, Jirani yao Shija amesimama amekwenda kuomba kama Sara binti wa Masanja anaweza akamsaidia kusoma taarifa muhimu kwa vile yeye na familia yake hawajui kusoma. Shuleni watoto wanapata ujuzi na maarifa ambayo wazazi hawayapati kama vile kusoma Mikataba, Lebo, Taarifa za uzalishaji, Maelezo ya muda wa matumizi, nk

**Swali:** **Je watoto wanaosoma maisha yao ya baadae yanaweza yakawaje?**

**Jibu:** Kwa elimu wanayoipata shuleni watoto wanaweza kuwasaidia wazazi wao kuboresha maisha yao, watoto wanaweza kutumia vipaji vyao kama watafanya kazi kwa bidii na baadae wakawa wataalamu wa kada mbalimbali kama vile Wakunga, Madaktari, Waandishi,Wahasibu au wataalamu wa kilimo.


PRIMARY AND SECONDARY SCHOOL
COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 12




**Swali: Unaona nini kwenye picha hii?**

**Jibu:** Ni muhula mpya wa masomo wanaonekana watoto wa Masanja wanafurahi kuwaona watoto wenzao wa Shija wakiwasili shuleni kwao.

**Swali: Nini kimebadilisha msimamo wa Shija na kuamua kuwapeleka watoto wake wakubwa wawili shuleni?**

**Jibu:** Shija amekuwa akiifuatilia kwa karibu familia ya Masanja kwa kipindi chote cha mwaka, Amegundua kuwa elimu hutoa fursa ya Maendeleo kwa watoto na familia kwa ujumla hasa katika Nyanja za Afya, Kuongeza mapato katika Kilimo,na kuongeza kipato katika ngazi ya familia. Shija ameona njia sahihi ya kuwekeza ni kupeleka watoto shule.


COTTON
MADE IN
AFRICA

# Picha Na 13




**Swali: Unaona nini kwenye picha hii?**

**Jibu:** Ni siku ya mapumziko watoto hawaendi shule, Watoto wa Masanja na Shija wanacheza michezo pamoja.

**Swali: Kwanini ni muhimu watoto kucheza michezo mbalimbali?**

**Jibu:** Watoto wana haki ya kucheza, Michezo ni muhimu kwa afya zao na maendeleo yao kwa ujumla.

# Aid by Trade Foundation

The Aid by Trade Foundation was created in 2005 by Dr. Michael Otto, an entrepreneur from Hamburg, Germany as an independent organization from the Otto Group. Its goal is to provide aid by trade for people to help themselves, thereby preserving vital natural resources and securing the livelihoods of future generations. The Aid by Trade Foundation is the umbrella organization of Cotton made in Africa and realizes its goals through this initiative.

**Imprint**

© **Aid by Trade Foundation**
Bramfelder Chaussee 105
22177 Hamburg
Germany
Tel.: +49 (0)40 - 6461 - 7971
Fax: ++49 (0)40 - 6461 - 1009
e-Mail: info@abt-foundation.org
www.cottonmadeinafrica.org

**Drawings:** Donald Grant, 2014
Printed with kind support of Systain Consulting